

KASIDA

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

KASIDA

Al-Qaseedah (Swahili Translation)
Tafsiri ya Kiswahili ya: KASIDA (Kiarabu)

Mtunzi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Karim-ud-Din Shams

Chapa ya Kwanza ya Aina Kamaalaate Islam ambamo ndani
yake imo kasida hii kwa Kiarabu: 1893
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2020

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:

Tanzania:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:

E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover Design by: Farhan Naseer

ISBN: 978-1-84880-528

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

NENO LA MWENEZAJI

Dawati la Kiswahili lina furaha kubwa kuwaletwa wasomaji wa Kiswahili tafsiri ya kasida ya Kiarabu iliyotungwa na Hadhrat Mwanzilishi^{as} wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kujaaliwa uwezo maalum na Mwenyezi Mungu.

Tumechapa tafsiri hii pamwe na matini ya Kiarabu ili wasomi wa Kiarabu nao wapate ladha yake kwa kuelewa jinsi kasida hii ilivyomsifu Mtume^{saw} kwa njia ngeni iliyoandikwa.

Twamshukuru Sheikh Karim-ud-Din Shams aliyebeba jukumu la kuifasiri kwa lugha ya Kiswahili. Kweli ametia bidii kubwa ili tuweze kuchangamka kwa kujua aliyotunga Seyidna Ahmad^{as} kwa Kiarabu kwa kumsifu Mtume Mteule^{saw}.

Kabla ya kupelekwa katika matbaa ili kuchapwa, niliidurusu kwa uangalifu kwa kuilinganisha na matini ya Kiarabu. Sheikh Ansar Hussain akasaidia kupanga herufi zake kwa kompyuta na kisha kutayarisha fometi yake.

Mwenyezi Mungu Awape malipo bora wote walioishughulikia kazi hii kwa njia yoyote. Mola wetu Awanu-faishe wasomaji wa kasida hii na tafsiri yake. Amin.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan

9 Machi 2020

KASIDA

Seyidna Ahmad^{as} ameandika kuhusu kasida yake ndani ya kitabu chake Aina Kamaalaate Islam yafuatayo:

“Kasida hii ni nadhifu na yenye jamala iliyojaa taaluma za fasihi na lulu zenye thamani zisizo na kifani za lugha ya Kiarabu, inayohusu kumsifu Bwana wangu na Mfalme wa dunia na Akhera, Khatam-un-Nabiyyin, Hadhrat Muhammad^{saw} ambaye amesifiwa na Allah ndani ya Kurani Tukufu. Ewe Mwenyezi Mungu, Umshushie baraka na amani hadi siku ya kiama. Na kasida hii haitokani na ujuzi wangu uliopoa na akili yangu isiyo kali; wala mawazo yangu makavu sio mpanda farasi hodari wa medani hii wala sio chimbuko la siri hizi za maarifa. Bali yote niliyosema, yametoka kwa Mola Wangu Ambaye ni Rafiki yangu na Msaidizi wangu, Ambaye Yuko nami kila wakati. Ndiye Anayenilisha na kuninyewesha. Na nipoteapo njia, Yeye Ananiongoza. Na niuguapo, Ananiponya. Nami sikujichumia kwa juhudi zangu maneno yoyote ya kuvutia na ya nadra, bali Mungu Akanijaalia ushindi juu ya walio mabingwa wa lugha. Na hii ni ishara kubwa ya Mola wangu kwa watu wenye ujuzi. Nami nimeidhihirisha na kuibainisha ili nijaaliwe malipo ya wenye shukurani, na ili nisijumuishwe pamoja na wale wasiotoa shukurani.” (*Aa’ina-e-Kamaalaat-e-Islam*, Ruhaani Khazaa’in, vol. 5, p. 590)

KASIDA

1. يَا عَيْنَ فَيْضِ اللَّهِ وَ الْعِرْفَانِ
يَسْغَى إِلَيْكَ الْخَلْقُ كَالظَّهَانِ

Ewe uliye chemchem ya fadhili na maarifa ya Allah!
Mahuluku wanakukimbilia kama mwenye kiu.

2. يَا بَحْرَ فَضْلِ الْمُنْعِمِ الْمَنَّانِ
تَهْوَى إِلَيْكَ الرُّمُرُ بِالْكِيزَانِ

Ewe bahari ya fadhili za mwenye kuneemesha na
kufanya hisani, makundi ya watu wanaharakia kwako na
vikombe vyao.

3. يَا شَمْسَ مُلْكِ الْحُسْنِ وَالْإِحْسَانِ
تَوَزَّتْ وَجْهَ الْبَرِّ وَالْعُبْرَانِ

Ewe jua la nchi ya uzuri na ihsani, umeangaza miji na
mapori.

4. قَوْمٌ رَأَوْكَ وَ أُمَّتُهُ قَدْ أُخْبِرَتْ
مِنْ ذَلِكَ الْبُذْرِ الَّذِي أَصْبَانِي

Kaumu moja imekuona na umati mwingine umepewa
habari za mwezi mpevu, aliyenifanya kuwa ashiki wake.

5. يَبْكُونَ مِنْ ذِكْرِ الْجَمَالِ صَبَابَةً
وَ تَأَلَّمُوا مِنْ لَوْعَةِ الْهَجَرَانِ

Wanalia kwa kukumbuka uzuri wako kwa huba nyingi,
na pia kwa kuumia kwa sababu ya kukaa mbali nawe.

6. وَ أَرَى الْقُلُوبَ لَدَى الْحَنَاجِرِ كُرْبَةً
وَ أَرَى الْغُرُوبَ تُسِيلُهَا الْعَيْنَانِ

Nami nazona nyoyo zimeshafika kwenye halkumu kwa
sababu ya kukosa utulivu, na ninaona macho
yakitiririsha machozi.

7. يَا مَنْ غَدَا فِي نُورِهِ وَ ضِيَائِهِ
كَالنَّيِّرَيْنِ وَ نَوَّرَ الْمَلَوَانَ

Ewe, ambaye kwa nuru yake na mwanga wake
umekuwa kama jua na mwezi; na usiku na mchana
umeng'arika.

8. يَا بَدْرَنَا يَا آيَةَ الرَّحْمَنِ
أَهْدَى الْهُدَاةِ وَ أَشْجَعَ الشُّجْعَانِ

Ewe Mwezi wetu Mpevu, Ewe ishara ya Rahmani,
Kiongozi wa viongozi wote, na shujaa kuliko mashujaa
wote!

9. إِنِّي أَرَىٰ فِي وَجْهِكَ الْمُتَهَلِّلِ
شَاثًا يَّفُوقُ سَمَائِلَ الْإِنْسَانِ

Kwa hakika naona katika uso wako ung'ao shani inayoshinda sifa njema za binadamu wote.

10. وَقَدْ اقْتَفَاكَ أُولُو التَّهْلِي وَبَصِدُ قِيهِمْ
وَدَعُوا تَذَكُّرَ مَعَهْدِ الْأَوْطَانِ

Na bila shaka wenye busara wamekufuata, nao wameacha hata kukumbuka watani wao kwa sababu ya uaminifu wao.

11. قَدْ اثْرُوكَ وَفَارَقُوا أَحْبَابَهُمْ
وَتَبَاعَدُوا مِنْ حَلَقَةِ الْإِخْوَانِ

Bila shaka walikutanguliza na kuwaacha marafiki zao, na kutengana na ndugu zao.

12. قَدْ وَدَّعُوا أَهْوَاءَ هُمْ وَنُفُوسَهُمْ
وَ تَبَرَّءُوا مِنْ كُلِّ نَشْبٍ فَإِنْ

Walijitanga na matamanio yao na nafsi zao, na waliondokewa na hamu ya miliki yenye kuangamia.

13. ظَهَرَتْ عَلَيْهِمْ بَيِّنَاتُ رَسُولِهِمْ
فَتَمَرَّقَ الْأَهْوَاءُ كَالْأَوْثَانِ

Dalili bayana za Mtume^{saw} wao zikawadhihirikia, basi tamaa zao zikavunjika tikitiki kama masanamu.

14. فِي وَقْتٍ تَرْوِيحِ اللَّيَالِي نُورُوا
وَاللَّهُ نَجَاهُكُمْ مِنَ الطُّوفَانِ

Katika wakati wa giza la mausiku wakaangazwa, na Allah Akawaokoa katika tufani.

15. قَدْ هَاضَهُمْ ظُلْمُ الْأَنْلَاسِ وَضَيُّهُمْ
فَتَتَبَّعُوا بِعِنَايَةِ الْمَنَانِ

Bila shaka dhulma za watu zikawaponda sana, lakini wakasimama kidete kwa rehema ya Manani.

16. نَهَبَ اللَّيَّامُ نُشُوبَهُمْ وَعِقَارَهُمْ
فَتَهَلَّلُوا بِجَوَاهِرِ الْفُرْقَانِ

Waovu walipora mali zao na miliki zao. Lakini wakachangamka kwa kupata lulu za Kurani.

17. كَسَحُوا بُيُوتَ نَفُوسِهِمْ وَ تَبَادَرُوا
لِتَمْتَحَ الْإِيْقَانِ وَالْإِيْمَانِ

Wakafagilia mbali taka za undani wa nafsi zao na wakaharakia kunufaika na yakini na imani.

18. قَامُوا بِأَقْدَامِ الرَّسُولِ بِغَزْوِهِمْ
كَالْعَاشِقِ الْمَشْغُوفِ فِي الْبَيْدَانِ

Pamoja na Mtume^{saw} kusonga mbele, wakasimama kidete kwenye vita vyao katika medani kama ashiki aliyelewa na mahaba.

19. فَدَمَ الرِّجَالِ لِصِدْقِهِمْ فِي حُبِّهِمْ
تَحْتَ السُّيُوفِ أُرِيقَ كَالْقُرْبَانِ

Basi damu za nguli, kwa uthabiti wao katika huba yao, zilimwagwa chini ya panga kama dhabihu.

20. جَاءُوكَ مَنُحُوبِينَ كَالْعُرْيَانِ
فَسَتَرْتَهُمْ بِمَلَاحِفِ الْإِيْمَانِ

Wakakujia kama rabana wakiishaporwa mali yao, nawe ukawavisha shuka za imani.

21. صَادَقْتُهُمْ قَوْمًا كَرُوتٍ ذِلَّةً
فَجَعَلْتُهُمْ كَسَيْبِكَةِ الْعُقَيَانِ

Uliwakuta duni kama kinyesi cha mnyama, ukawafanya kuwa bongwe la dhahabu halisi.

22. حَتَّىٰ انْتَلَىٰ بُرُكَيْلَ حَدِيقِهِ
عَذْبِ الْمَوَارِدِ مُشِيرِ الْأَغْصَانِ

Hata nchi kavu ikawa kama bustani yenye chemchem ya maji baridi na matawi yaliyojaa matunda.

23. عَادَتْ بِلَادُ الْعُرَبِ نَحْوَ نَضَارَةٍ
بَعْدَ الْوَلَجِ وَالْمَحَلِّ وَالْحُسْرَانِ

Nchi ya Arabuni ikarutubika baada ya ukavu, ukame na uharibifu.

24. كَانَ الْحِجَازُ مَغَازِلَ الْغَزَلَانِ
فَجَعَلْتُهُمْ فَايِنَ فِي الرَّحْمَانِ

Wenyeji wa Hijazi walikuwa wamejishughulisha katika ashiki ya wanawake wenye macho ya kuvutia, nawe ukawafanya kuwa wenye kujifia katika mapenzi ya Rahmani.

25. شَيْئَانِ كَانَ الْقَوْمُ عُمِيًّا فِيهِمَا
حَسُو الْعَقَارِ وَ كَثُرَةُ الدِّسْوَانِ

Kulikuwa na mambo mawili ambayo kaumu hii ilikuwa imeyashughulikia kwa kupindukia: kunywa pombe na wanawake wengi.

26. أَمَّا النِّسَاءُ فَحَرِّمْتُ إِنْكَاحَهَا
زَوْجًا لَهُ التَّحْرِيمُ فِي الْقُرْآنِ

Ama wanawake, basi ilipigwa marufuku kuolewa kwao kwa mume aliyeharamishwa ndani ya Kurani.

27. وَجَعَلْتُ دُسْكَرَةَ الْهَدَامِ مُحَرَّبًا
وَ أَزَلْتُ حَائَتَهَا مِنَ الْبُلْدَانِ

Ulivifanya ukiwa vilabu vya pombe na kuyaondolea mbali mijini maduka ya kileo.

28. كَمْ شَارِبٍ بِالرَّشْفِ دَنَّا طَافِحًا
فَجَعَلْتَهُ فِي الدِّينِ كَالنَّشْوَانِ

Wengi walioje waliokuwa wanagugumia pombe vikombe baada ya vikombe, nawe ukawafanya kama waliolewa katika huba ya dini.

29. كَمْ مُحَدِّثٍ مُسْتَنْطِقِ الْعَيْدَانِ
قَدْ صَارَ مِنْكَ مُحَدِّثَ الرَّحْمَنِ

Kuna wengi wenye bidaa waliokuwa wapiga fidla wakawa wenye kuongolewa na Rahmani kwa kulelewa nawe.

30. كَمْ مُسْتَهَامٍ لِلرُّشُوفِ تَعَشُّقًا
فَجَذَبَتْهُمْ جُذْبًا إِلَى الْفُرْقَانِ

Wengi walioje waliowahangaikia katika ashiki vipusa wenye vinywa vinukiavyo, nawe ukawavutia kwenye Furqani (Kurani Tukufu).

31. أَحْيَيْتَ أَمْوَاتَ الْقُرُونِ بِجُلُوءِ
مَاذَا يُمِثِّلُكَ بِهَذَا الشَّانِ

Ukawafufua wafu wa karne nyingi kwa onyesho moja tu la utukfu. Ni nani awezaye kuwa mithili yako katika shani hii!

32. تَرَكُوا الْغُبُوقَ وَبَدَّلُوا مِنْ ذَوْقِهِ
ذَوْقَ الدُّعَاءِ بِلَيْلَةِ الْأَحْزَانِ

Wakaachilia mbali pombe ya jioni na kubadili ladha yake kwa ladha ya ibada ya usiku wa majonzi.

33. كَانُوا بِرَثَاتِ الْمَثَانِ قَبْلَهَا
قَدْ أَحْصَرُوا فِي شُجَّهَا كَالْعَانِ

Hapo kabla walikuwa kama wafungwa wa tamaa ya lahani za gitaa yenye nyuzi mbili.

34. قَدْ كَانَ مَرَّتَهُمُ أَغَانِي دَائِمًا
طَوْرًا بَغِيْدٍ تَارَةً بِدِيَانِ

Walikuwa wanajishughulisha na miziki muda wote, mara kwa warembo wenye ngozi nyororo na mara kwa mitungi ya pombe.

35. مَا كَانَ فِكْرٌ غَيْرِ فِكْرِ غَوَانِي
أَوْ شُرْبِ رَاحٍ أَوْ خِيَالِ جِفَانِ

Hawakufikiria kitu isipokuwa kufikiria wanawake warembo au kunywa pombe au kuzama katika fikara za vikombe vya kileo.

36. كَانُوا كَمَشْغُوفِ الْفَسَادِ بِجَهْلِهِمْ
رَاضِينَ بِالْأَوْسَاحِ وَالْأَكْدَرَانِ

Kwa ujinga wao, kama mwenye kupenda kupindukia ufisadi, wakaridhika na uchafu na taka.

37. عَيَّانٍ كَانَ شِعَارُهُمْ مِنْ جَهْلِهِمْ
مُحَقُّ الْحِمَارِ وَ وَثْبَةُ السَّرْحَانِ

Aibu mbili zilikuwa ni utambulisho wao: ukaidi wa punda na ushambuliaji wa mbwamwitu.

38. فَطَلَعْتَ يَا شَمْسَ الْهُدَى نُصْحًا لَهُمْ
لِتُضِيَّيَهُمْ مِنْ وَجْهِكَ التُّورَانِي

Basi, Ewe jua la mwongozo! Ulijitokeza kwa kuwahurumia ili uwaangaze kwa uso wako ung'aa.

39. أُرْسِلْتُ مِنْ رَبِّ كَرِيمٍ مُحْسِنٍ
فِي الْفِتْنَةِ الصَّبَاءِ وَالطُّغْيَانِ

Ulitumwa na Mola Mkarimu, Mhisani, wakati wa fitina kubwa na uasi.

40. يَا لَلْفَتَى مَا حُسْنُهُ وَ جَمَالُهُ
رَيَّاهُ يُضَيِّ الْقَلْبَ كَالرَّيْحَانِ

Aa, kijana huyu! ulioje uzuri wake na jamala yake. Harufu yake nzuri inauvutia moyo kama mrehani.

41. وَجْهَ الْمُهَيَّبِينَ ظَاهِرٌ فِي وَجْهِهِ
وَشُؤْنُهُ لَبَعَثَ بِهَذَا الشَّانِ

Uso wa Mwenyezi Mungu unadhirika katika uso wake na sifa za Mungu zikamulika katika shani yake hii.

42. فَلَذَا يُحِبُّ وَ يَسْتَحِقُّ بِجَمَالِهِ
شَغَفًا بِهِ مِنْ زُمْرَةِ الْأَخْدَانِ

Kwa hiyo yuapendwa, na uzuri wake unastahiki kwamba yeye apendwe sana kutoka katika kundi la marafiki.

43. سُجَّحَ كَرِيمٌ بِإِذْلِ خُلِّ الثَّقَى
خِرْقٌ وَفَاقَ طَوَائِفَ الْفِتْيَانِ

Yu mwenye huluka bora, mheshimiwa, mkarimu, rafiki wa kweli wa uchamungu, mpaji, na amewapita mashujaa wote.

44. فَاقَ الْوَرَى بِكَمَالِهِ وَجَمَالِهِ
وَ جَلَالِهِ وَ جَنَانِهِ الرَّيَّانِ

Yeye amewapita mahuluku wote kwa ukamilifu wake na uzuri wake na utukufu wake na moyo wake laini.

45. لَا شَكَّ أَنَّ مُحَمَّدًا خَيْرُ الْوَرَى
رَيْقُ الْكِرَامِ وَنُحْبَةُ الْأَعْيَانِ

Bila shaka yoyote Muhammad^{saw} ni mbora wa mahuluku mwenye fadhila baina ya waheshimiwa, na mteule kati ya viongozi.

46. تَمَّتْ عَلَيْهِ صِفَاتُ كُلِّ مَرِيَّةٍ
خُتِمَتْ بِهِ نِعْمَاءُ كُلِّ زَمَانٍ

Sifa za kila fadhila zimeishia kwake na neema za kila zama zimeishia kwake yeye.

47. وَاللَّهِ إِنَّ مُحَمَّدًا كَرِذَافَةٍ
وَبِهِ الْوُصُولُ بِسُدَّةِ السُّلْطَانِ

Wallahi! Muhammad^{saw} ni kama naibu wake (Allah Mtukufu), na kwa kupitia yeye tu kwaweza kuingia barazani mwa Sultani.

48. هُوَ فَخْرُ كُلِّ مُطَهَّرٍ وَ مُقَدَّسٍ
وَ بِهِ يُبَاهَى الْعَسْكَرُ الرُّوحَانِي

Yu fahari ya kila aliyetakaswa na aliyetukuka, na Jeshi la kiroho linafahiri kwake.

49. هُوَ خَيْرُ كُلِّ مُقَرَّبٍ مُتَقَدِّمٍ
وَ الْفَضْلُ بِالْخَيْرَاتِ لَا بِزَمَانٍ

Yu mbora kuliko kila aliyejaaliwa ukaribu na Mungu na kuliko aliyesonga mbele. Na fadhila hutegemea matendo mema sio zama.

50. وَالظُّلُّ قَدْ يَبْدُو أَمَامَ الْوَابِلِ
فَالظُّلُّ ظُلٌّ لَيْسَ كَالظُّهُتَانِ

Pengine inanyunya kabala ya mvua kubwa, na manyunyuyu ni mayunyuyu tu, sio kama mvua kubwa.

51. بَطْلٌ وَحِيدٌ لَا تَطِيْشُ سِهَامُهُ
ذُو مُضْمِيَّاتٍ مُؤَبِّقِ الشَّيْطَانِ

Yeye ni shujaa pekee ambaye mishale yake haikosi shabaha. Yu mwenye mishale inayolenga shabaha barabara, ndiye mwenye kumuangamiza shetani.

52. هُوَ جَنَّةٌ إِنِّي أَرَى أُنْمَارَهُ
وَ قُطُوفَهُ قَدْ ذُلِّلَتْ لِجَنَانِي

Yu bustani. Naona matudna yake, na matawi yake yaliyojaa matunda yameneseshwa kwa ajili ya moyo wangu.

53. أَلْفَيْتُهُ بَحْرَ الْحَقَائِقِ وَ الْهُدَى
وَ رَأَيْتُهُ كَالدُّرِّ فِي اللَّبْعَانِ

Nimemkuta kuwa bahari ya mambo ya kweli na mwongozo. Na nimemwona katika mng'ao ni kama lulu.

54. قَدْ مَاتَ عِيسَى مُطْرِقًا وَ نَبِيُّنَا
حَيٌّ وَ رَبِّي إِنَّهُ وَافَانِي

Isa^{as} akiinama kichwa chake amekwishafariki, na Mtume^{saw} wetu yu hai. Wallahi yeye^{saw} amekutana nami.

55. وَ اللَّهُ إِلَيَّ قَدْ رَأَيْتُ بِجَالِهِ
بِعُيُونٍ جَسَمِي قَاعِدًا بِمَكَانِي

Wallahi! Mimi nimeona uzuri wake kwa machao yangu ya kimwili nikiwa nimekaa mahala pangu.

56. هَا إِنْ تَظَلَّيْتُ ابْنَ مَرْيَمَ عَائِشًا
فَعَلَيْكَ إِنْجَابًا مِنْ الْبُؤْهَانِ

Tazama! Kama wewe unadhani kuwa mwana wa Mariamu yu hai, basi ni juu yako kuthibitisha kwa hoja.

57. أَفَأَنْتَ لَأَقَيْتَ الْمَسِيحَ بِبِقْطَةٍ
أَوْ جَاءَكَ الْأَنْبَاءُ مِنْ يَقْطَانَ

Je, umeonana na Masihi ukiwa macho? Au zimekujia habari kutoka kwa aliye macho?

58. أَنْظُرْ إِلَى الْقُرْآنِ كَيْفَ يُبَيِّنُ
أَفَأَنْتَ تُعْرِضُ عَنْ هُدَى الرَّحْمَنِ

Itazame Kurani jinsi inavyobainisha (kifo chake). Je unaupa kisogo mwongozo wa Rahmani?

59. فَاعْلَمْ بِأَنَّ الْعَيْشَ لَيْسَ بِثَابِتٍ
بَلْ مَاتَ عَيْسَى مِثْلَ عَبْدٍ فَإِنْ

Basi ujue kuwa uhai wake hauthibitiki, bali Isa^{as} ameshafiriki dunia mithili ya mtu ajifiaye.

60. وَ نَبِيِّنَا حَيٌّ وَ إِيَّاهُ شَاهِدٌ
وَ قَدْ افْتَكَفْتُ قَطَائِفَ اللُّغَيَانِ

Na Nabii wetu^{saw} yuko hai, nami ni shahidi, na mimi nimekonyoa matunda ya kumlaki.

.61
وَ رَأَيْتُ فِي رَيْعَانٍ عُمْرِي وَجْهَهُ
ثُمَّ النَّبِيُّ يِقْطَعُنِي لِقَائِي

Nilimwona uso wake katika ujana wangu, tena
Mtume^{saw} akakutana nami nikiwa macho.

.62
إِنِّي لَقَدْ أُحْيَيْتُ مِنْ إِحْيَائِهِ
وَأَهَا لِإِعْجَازٍ فَمَا أَحْيَانِي

Hakika nimepata kuhiika kwa sababu yeye kunihuisha.
Nastaajabia muujiza huu! Ajabu ilioje yeye kunihuisha!!

.63
يَا رَبِّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّكَ دَائِمًا
فِي هَذِهِ الدُّنْيَا وَ بَعَثْ ثَانٍ

Ewe Mola wangu! Umteremshie baraka Nabii wako
daima dwamu katika dunia hii na huko Akhera.

.64
يَا سَيِّدِي قَدْ جِئْتُ بِأَبْكَ لَاهِفًا
وَ الْقَوْمُ بِالْإِكْفَارِ قَدْ أَدَانِي

Ewe Bwana wangu! Nimefika mlangoni pako nikiwa na
majonzi, ilhali kaumu imeniudhi kwa kunikufurisha.

65. يَفْرِى سِهَامَكَ قَلْبَ كُلِّ مُحَارِبٍ
وَ يَشُجُّ عَزْمَكَ هَامَةَ الثُّعْبَانِ

Mishale yako huchoma moyo wa kila mpiganaji wa vita,
na azimio yako yaponda kichwa cha chatu.

66. اللَّهُ ذُرُّكَ يَا إِمَامَ الْعَالَمِ
أَنْتَ السَّبُوقُ وَ سَيِّدُ الشُّجْعَانِ

Heri yako yote hutoka kwa Mungu, Ewe Imamu wa
walimwengu wote. Umewapita wote, u kiongozi wa
mashujaa wote.

67. أَنْظِرْ إِلَى بَرَحْمَةِ وَ تَحْنٍ
يَا سَيِّدِي أَنَا أَحَقُّرُ الْعِلْمَانِ

Niangalie kwa huruma na upole, Ewe Bwana wangu!
Mimi ni mtumishi wako mnyonge.

68. يَا حَبِّ إِنَّكَ قَدْ دَخَلْتَ مَحَبَّةً
فِي مُهَجَّتِي وَ مَدَارِكِي وَ جَنَانِي

Ewe mpendwa wangu, wewe umeingia kimapenzi katika
roho yangu, hisia zangu na moyo wangu.

69. مِنْ ذِكْرِ وَجْهِكَ يَا حَدِيقَةَ بَهْجَتِي
لَمْ أَخُلْ فِي لَحْظٍ وَلَا فِي أَنْ

Ewe bustani ya furaha yangu! sighafiliki wakati wowote hata kidogo kukumbuka uso wako.

70. جَسْبِي يَطِيرُ إِلَيْكَ مِنْ شَوْقٍ عَلَا
يَا لَيْتَ كَأَنْتَ قُوَّةُ الطَّيْرَانِ

Mwili wangu unataka kuruka kukujia kwa shauku kubwa. Laiti ningekuwa na uwezo wa kuruka!